

TAARIFA KWA UMMA

MATUMIZI SALAMA YA MITUNGI YA GESI

Sheria ya Mafuta ya Petroli, Sura ya 392 (The Petroleum Act, Cap 392), inaipa EWURA mamlaka ya kusimamia na kutoa mwongozo wa namna bora ya kutoa huduma pasipo kuathiri mazingira, usalama wa watu na mali zao. Hivi karibuni EWURA imebaini kushamiri kwa mitungi ya gesi ambayo ni ya zamani, yenye zaidi ya miaka 30 ikitumika katika kujazwa gesi na kuuzwa maeneo mbalimbali nchini. Mitungi hiyo hajakaguliwa rasmi wala kuidhinishwa kuwa ni salama kwa matumizi. Kiusalama, mitungi hii ya gesi haipaswi kutumika kwa sababu inahatarisha usalama wa watumiaji, mali zao na umma kwa ujumla.

EWURA inawatahadharisha wauzaji wa gesi wa rejareja kuacha mara moja kutumia mitungi ya gesi ambayo imepigwa marufuku na ambayo haijafanyiwa ukaguzi kuhakiki usalama wake kama inafaa kutumika. Mitungi iliyokaguliwa lazima ipate idhini ya Kampuni inayoagiza gesi nchini.

Yeyote mwenye mitungi ya gesi ya zamani na isiyokaguliwa anaagizwa kuirudisha kwa kampuni husika mara moja.

Makampuni yote yanayofanya biashara ya gesi ya kupikia nchini yanaagizwa kuhakikisha mitungi yao imefanyiwa ukaguzi kutathmini ubora na usalama wa mitungi hiyo kabla ya kuijaza. EWURA itafanya ukaguzi wa kushtukiza na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayekutwa na mitungi chakavu.

Limetolewa na:

MKURUGENZI MKUU

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI